

Kuwalisha kuku

Walishe kuku kulingana na umri.

Chakula cha kuku wa kutaga kinastahili kuwa na maganda ya chaza ya kilo 2- 3 kwa kila kilo 100.



Kuku wa kutaga wakila chakula



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Ojowi, M na Okoko, N

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kisii

S.L.P. 523, Kisii, 40200

Simu: (058)31800/1/2/3 au (058)31800

Baruapepe: kari-kisii@westernet.co.ke

Kisii-kari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 65 / 2008

Shilingi 20 za Kenya

Tumia keki ya mbegu za alizeti kama kiungo cha lishe ya mifugo



Utangulizi

Keki ya mbegu za alizeti iko na protini nyingi na inaweza kutumiwa kutengeneza lishe ya mifugo bila kutegemea vyakula vya dukani.

Keki hiyo inatumika kama nyongeza ya protini katika chakula cha ng'ombe au kuku.

Mazao ziada ya alizeti

Kilo 3.5 za mbegu za alizeti zilizosagwa hutoa lita moja ya mafuta na kilo 2.5 za keki ya mbegu.



Bidhaa zinazotoka kwa alizeti

Utengenezaji wa lishe shambani

I) Chakula cha ng'ombe wa maziwa

- Changanya kilo 18 za keki ya alizeti na kilo 100 za makapi ya mahindi kutengeneza chakula ya kuongeza maziwa ya ng'ombe.



Kuchanganya mahindi na keki ya alizeti

- Changanya kapi za mahindi na keki ya alizeti.
- Wapatie ng'ombe nyasi ya 'Napier' hadi washibe kisha lishe ya mseto wa alizeti. Wenya kiwango cha chini za maziwa, wapatie kilo 2, na wenye kiwango cha juu wapatie kilo 4.



Ng'ombe aliyelishwa vizuri

Ng'ombe aliyelishwa vizuri

i) Chakula cha mwanzo cha kuku

Changanya kilo 22 za keki ya alizeti pamoja na kilo 100 za makapi ya mahindi.

ii) Chakula cha ukuzaji

Changanya kilo 20 za keki ya alizeti na kilo 100 za makapi ya mahindi.

iii) Kuku wenye kutaga

Changanya kilo 18 za keki ya alizeti na kilo 100 za makapi ya mahindi.